# JARIDA LA SEKTA YA MADINI MKOANI RUVUMA






**OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA    JUNI 2020**

# YALIYOMO

**1.0 UTANGULIZI ........................................................2**

**2.0 SHUGHULI ZA UCHIMBAJI WA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA 3**

2.1 Utafiti wa Madini ya Urani ................................................ 4
2.2 Uchimbaji wa Madini ya Dhahabu .................................. 4
2.3 Uchimbaji wa Madini ya Vito vya Thamani ...................... 4
2.4 Uchimbaji wa Makaa ya Mawe ......................................... 5
2.5 Uchimbaji wa Madini ya Ulanga ....................................... 6
2.6 Uchimbaji wa Madini ya Shaba ........................................ 6
2.7 Uchimbaji mdogo wa Madini Mengineyo ......................... 7

**3.0 MASOKO YA MADINI ............................................7**

3.1 Umuhimu wa Masoko ya Madini ...................................... 8

**4.0 MFUMO WA UTOAJI WA LESENI ............................8**

**5.0 MFUMO WA ADA NA TOZO ZA SERIKALI KATIKA SHUGHULI ZA UCHIMBAJI NA BIASHARA YA MADINI ...................................9**

**6.0 KWA NINI UWEKEZE MKOANI RUVUMA??? .......10**

6.1 Upatikanaji wa Wafanyakazi na wachimbaji wenye ujuzi; 11
6.2 Uwepo wa miundombinu ya barabara zinazopitika kwa mwaka mzima 11
6.3 Upatikanaji wa Huduma Muhimu za Jamii .................... 11
6.4 Umilikishwaji wa ardhi ya uchimbaji madini ................. 12

**7.0 FURSA ZA UWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA ........................................................12**

**Kiambatisho Na. 1 ......................................................14**

Majukumu na Kazi za Ofisi ya Madini Mkoani Ruvuma 14

**Kiambatisho Na. 2 .......................................................**

Viwango vya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye Sekta ya Madini 15

# 1.0 UTANGULIZI

**Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa iliyopo Kusini mwa Tanzania ikipakana na Mkoa wa Njombe na Morogoro kwa upande wa Kaskazini; Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa upande wa Mashariki; nchi ya Msumbiji upande wa Kusini; na nchi ya Malawi upande wa Magharibi. Mkoa wa Ruvuma una idadi ya watu 1,376,891. kwa mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka 2012.**

**Mkoa wa Ruvuma una utajiri mkubwa wa rasilimali ya madini ambayo inahitaji uwekezaji ili kuweza kuchangia Pato la Taifaipasavyo. Ikiwa sekta ya madini itaendelezwa, kwa kuhamasisha uchimbaji wenye kutumia nyenzo na teknolojia ya kisasa uchumi wa mkoa utaimarika kutokana na hazina hiyo ya madini.**

**Madini yanayopatikana katika mkoa wa Ruvuma kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali Na. 1.ni pamoja na madini ya urani, dhahabu, shaba, vito vya thamani, ulanga,Chuma,Makaa ya mawe,Chokaa na madini ya ujenzi.**

| Aina ya madini | Kijiji | Wilaya |
|---|---|---|
| Dhahabu | Darpori, Mpepo, Liparamba, Mipotopoto, Nindi | Nyasa |
| | Lukarasi, Mhongozi | Mbinga |
| | Kitanda | Namtumbo |
| Urani *(Uranium)* | Likuyuseka–Maganga | Namtumbo |
| Shaba | Mbesa, Mbati | Tunduru |
| | Lukarasi, Mhongozi | Mbinga |
| Makaa ya mawe*(Coal)* | Ruanda, Mbuyula, Paradiso | Mbinga |
| | Mbambabay, Liweta | Nyasa |
| | Mhukuru, Mtyangimbole | Songea Vijijini |
| Chokaa *(limestone)* | Maposeni, Mtyangimbole | Songea Vijijini |
| Chuma | Mtonya | Namtumbo |
| *Ruby, Quartz* | Muhuwesi | Tunduru |
| *Tantalite* | Kiburungutu | Namtumbo |
| *Sapphire, Amethyst, Alexandrite, Tourmaline, Garnets, Aquamarine, Spinel* | Ngapa, muhuwesi, Mtetesi, Ngatala, Ligunga, Majimaji, Nakapanya na Lu-mesule | Tunduru |
| Ulanga | Kiburungutu | Namtumbo |
| Madini Ujenzi | Vijiji Vyote | Wilaya Zote - |

# 2.0 SHUGHULI ZA UCHIMBAJI WA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA

## 2.1 Madini ya Urani



**Katika Mkoa wa Ruvuma, madini ya urani yanapatikana katika Kata ya Likuyuseka–Maganga wilayani Namtumbo.Taarifa za awali za utafiti zilizofanyika kwenye maeneo ya Mkuju wilayani Namtumbo zilibaini kuwepo kwa mashapo ya madini ya urani kiasi cha Tani 16,284.**

**Taratibu za kuweza kuanza kuchimbwa kwa madini hayo zinaendelea na zipo katika hatua za mwisho.**

**Kampuni ya MANTRA tayari imepewa kibali yaani Envronment Impact Certificate cha Baraza la mazingira la Taifa NEMC ili waanze kazi ya kuchimba madini hayo ndani ya pori la Selous ambapo uchimbaji huo hadi kukamilika unatarajia kuchukua miaka 12.**

## 2.2 Uchimbaji wa Madini ya Dhahabu




**Utafiti na uchimbaji wa madini ya dhahabu katika Mkoa wa Ruvuma unafanyika katika Wilaya ya Nyasa (maeneo ya Darpori, Mpepo, Liparamba,Mipotopoto na Nindi);**

**Wilaya ya Mbinga (maeneo ya Lukarasi na Muhongozi); na Wilaya ya Namtumbo (eneo la Kitanda). Uzalishaji wa madini ya dhahabu katika mkoa wa Ruvuma uko chini ya kiwango kutokana na teknolojia na nyenzo duni zinazotumika katika shughuli za uchimbaji wa madini hayo.**



# 2.3 Uchimbaji wa vito vya thamani




**Madini ya vito vya thamani hupatikana maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Ruvuma.**

**Aina ya madini ya vito vya thamani yanayopatikana Mkoa wa Ruvuma nipamoja na *Ruby, Sapphire, tantalite, Aquamaline,quartz, Amethyst,Alexandrite,Garnets na Spinel.* Shughuli za uchimbaji ya vito vya thamani zinafanyika katika wilaya za Mbinga. Songea, Tunduru na Namtumbo kwenye maeneo yaliyobainishwa katika Jedwali Na.1**

**Wilaya ya Tunduru ni moja ya wilaya yenye aina nyingi za madini ya vito vya thamani na hivyo hutoa fursa ya uwekezaji kwa uchimbaji madini hayo.**

**Katika kuimarisha uchimbaji wa madini hayo, Tume ya Madini inaratibu zoezi la kutenga eneo la Ngapa lenye ukubwa wa hekta 7548.5 kwa ajili ya uchimbaji mdogo wa madini.**



# 2.4 Uchimbaji wa makaa ya mawe




**Shughuli za utafiti na uchimbaji wa makaa ya mawe katika mkoa wa Ruvuma zinafanyika katika Wilaya ya Mbinga (maeneo ya Mbalawala na Mbuyula);**

**Wilaya ya Songea (maeneo ya Muhukuru, Njuga na Mtyangimbole) na Wilaya ya Nyasa (maeneo ya Mbambabay na Nyasa) kama inavyooneka kwenye Ramani Na.1.**



**Taarifa za tafiti za awali za makaa ya mawe katika maeneo ya Mbalawala nitani milioni 99.5; Mbuyula tani milioni 15.1; Muhukuru tani milioni 27; Njuga tani milioni 23; Mbambabay tani milioni 29; Liweta tani milioni 34. Ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana kwenye maeneo hayo yana wastani wa Calorific Value (CV)**

# *Ramani 1: Hazina ya Mashapo ya Makaa ya Mawe katika Mkoa wa Ruvuma*




**Uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe unafanyika katika maeneo ya Mbalawala, Mbuyula, Mbambabay, Muhukulu na Liweta.**

**Wateja wakubwa wa makaa ya mawe yanayochimbwa katika maeneo hayo kwa sasa wapo ndani ya nchi na katika nchi jirani za Rwanda, Kenya na Uganda.**

**Makaa ya mawe yanayozalishwa na kuuzwa kwenye masoko hayo ni kiasi cha wastani wa tani 55,000 kwa mwezi ambapo kati ya kiwango hicho asilimia 70% yanauzwa ndani ya nchi.**

**Hazina ya makaa ya mawe yaliyopo kwenye maeneo hayo inakadiriwa kuwa ziadi ya Tanimilioni 227.6 ambapo uzalishaji unaofanyika kwa sasa wa wastani wa Tan 55,000 utachukua takribani miaka zaidi ya 300 kumaliza hazina hiyo.**

**Mataifa mengine yaliyoonesha nia ya kununua makaa yamawe yanayochimbwa katika maeneo hayo ni pamoja na India na China.**

# 2.5 Uchimbaji wa madini ya Ulanga



**Madini ya Ulanga *(mica)* ni kundi la madini laini yanayopatikana yakiwa na umbo bapa.**



**Madini hayo yanapatikana katika maeneo ya Kijiji cha Kiburungutu Wilayani Namtumbo. Madini haya hutumika kwa wingi katika teknolojia ya kielektroniki kama kihami umeme (resistor) katika utengenezaji wa *capacitor*. na utehutumiwa sana ndani ya kapasita.**

**Uchimbaji unaofanyika katika maeneo yenye mashapo ya madini hayo ni uchimbaji mdogo.**

# 2.6 Uchimbaji wa madini ya shaba



**Madini ya shabayanayopatikana katika Mkoa wa Ruvuma ni yale yaliyo na rangi ya bluu ambapo yanapatikana kwa wingi katika maeneo ya Mbesa - Nalasi wilayani Tunduru.**




**Madini ya shaba ya bluu yana thamani kuzidi madini ya shaba aina nyingine zote ikiwemo shaba nyekundu ambayo inachimbwa katika nchi jirani ya Zambia. Kugundulika kwa madini hayo kunaifanya wilaya ya Tunduru kuwa ndiyo wilaya pekee nchini na Afrika mashariki na kati kuwa na madini ya shaba ya bluu.**

**Utafiti wa awali wa kijiolojia uliofanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1988 na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), katika eneo la Kata ya Mbesa wilayani Tunduru, ulibaini kuwepo kwa madini mengi aina ya shaba ya bluu.**

# 2.7 Uchimbaji mdogo wa madini mengineyo




**Pamoja na juhudi za utafiti na uchimbaji wa madini kama ilivyobainishwa hapo juu, Mkoa wa Ruvuma, umebarikiwa pia kuwa na madini aina ya *Tantalum* ambayo ni mojawapo ya madini yaliyopo kwenye kundi la 3T's mengine yakiwa *Tin* na *Tungsten*.**

**Madini hayo ya *Tantalum* yanapatikana katika maeneo ya Kijiji cha Kiburungutu wilayani Namtumbo.**



**Mkoa wa Ruvuma una hazina ndogo ya madini ya viwandani kama Chokaa yanayopatikana katika eneo la kijiji cha Mtyangimbole wilayani Songea. Aidha madini ya chuma yanapatikana katika eneo la Mtonya wilayani Namtumbo, Madini ya ujenzi kama kokoto, mchanga na kifusi hupatikana katika maeneo mengi ya mkoa wa Ruvuma.**

# 2.8 Masoko ya madini




**Masoko ya Madini ya dhahabu na vito vya thamani katika mikoa yameanzishwa kwa mujibu wa THE MINING (MINERAL AND GEM HOUSES) REGULATIONS, 2019.**

**Mkoa wa Ruvuma una masoko mawili ya Madini ambayo ni Soko la Madini Songea, na Soko la Madini Tunduru. Malengo ya kuanzishwa kwa masoko ya madini katika sekta ya madini ni pamoja na kuongeza uwazi; utangazaji; usawa; mwendelezo; na ulinzi wa haki halali na masilahi ya watu wanaofanya biashara.**

**Zaidi ya kilogramu 42 za dhahabu na kilogramu 340 za madini ghafi ya vito vya thamani yameuzwa katika masko ya madini mkoa wa Ruvuma katika kipindi cha Mei 2019 hadi Mei 2020.**

**Wauzaji wakuu wa madini katika masoko ya madini yaliyopo mkoa wa Ruvuma ni wachimbaji wadogo pamoja na wafanyabiashara wenye leseni za udalali wa madini ambapo wafanyabiashara wakubwa *(Dealers)* wamekuwa ndio wanunuzi wa madini hayo sokoni.**

## 2.9 Umuhimu wa masoko ya madini




**Faida za uanzishwaji wa masoko ya madini nchini ni pamoja na:**

**Wachimbaji wa madini kupata bei nzuri ya madini kutokana na uwazi uliopo sokoni;**

**Wachimbaji wa madini kutokuwa na haja ya kutorosha madini, kitendo ambacho kilikuwa ni hatari kwani kilikuwa kinasababisha wachimbaji kupokonywa madini yao na serikali pamoja na kukabiliwa na kifungo pindi wanapobainika kutenda kosa hilo;**

**Serikali kupata takwimu sahihi za mauzo ya mazini na urahisi wa kukusanya mapato yaliyokuwa yakipotea kutokana na utoroshaji wa madini;**

**Kuongezeka kwa tija ya utendaji kazi kwenye ofisi za madini kutokana na watumishi wa ofisi hizo kufanya shughuli nyingine badala ya kupoteza muda mwingi kuwafuatilia wachimbaji wa madini migodini;**

**Serikali kupata takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya madini nchini; na**

**Kuongezeka kwa mapato ya serikali yatokanayo na shughuli za uchimbaji na biashara ya madini.**

# 3.0 Mfumo wa utoaji leseni

**Tume ya Madini imeundwa kutokana na maboresho yaliyofanyika mwaka 2017 katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010.**

**Tume ya madini imepewa mamlaka na majukumu (Kiambatisho Na. 1) ya kusimamia sekta ya madini nchini. Ofisi za Afisa Madini Mkazi zilizopo mikoani zinatekeleza majukumu hayo ya Tume katika kusimamai sekta ya Madini katika ngazi ya Mkoa.**

**Mojawapo ya jukumu la Tume ya Madini ni kutoa leseni mbalimbali zinazohusiana na shughuli za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na biashara ya Madini. Jedwali Na. 2 linaonesha makundi mbalimbali ya leseni zinazotolewa naTume ya Madini.**

***Jedwali Na. 2: Makundi ya Leseni zinazotolewa na Tume ya Madini***

| **Kundi** | **Daraja** | **Aina ya Leseni** | Size /Area | Capital |
|---|---|---|---|---|
| Leseni za Uchimbaji | A | i. Prospecting licence (PL) | | |
| | | ii. Gemstone prospecting licence (GPL) | | |
| | | iii. Retention licence (RL) | | |
| | B | i. Special mining licence (SML) | | |
| | | ii. Mining licence (ML) | | |
| | C | i. Primary mining licence (PML) | | |
| | D | i. Processing licence (PCL) | | |
| | | ii. Smelting licence (SL) | | |
| | | iii. Refining licence (RFL) | | |
| Leseni za biashara ya madini | Biashara kubwa ya Madini (Dealer licence) | | | |
| | Biashara ya Udalali wa Madini (Broker License) | | | |
| Uchenjuaji Madini (Processing) | | | | |
| Uyeyushaji wa Madini (Smelting) | | | | |
| Usafishaji wa Madini (Refinery) | | | | |

## 3.1 MFUMO WA ADA NA TOZO ZA SERIKALI KATIKA SHUGHULI ZA UCHIMBAJI NA BIASHARA YA MADINI

**Kufuatia maboresho yaliyofanywa mwaka 2017 kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, imebainisha viwango vya mrabaha na ada za vibali vya kuingiza (import) na kutoa (export) madini nchini ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3 na 4.**
**Aidha, ada na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake ya Mwaka 2017 ni kama zinavyoonekana kwenye Kiambatisho Na. 2.**

***Jedwali Na. 3 Viwango vya Mrabaha na Ada ya Ukaguzi kwa Mauzo ya Madini***

| ***Aina ya Madini*** | ***Kima cha Mrabaha*** |
|---|---|
| *Urani* | *6%* |
| *Almasi, Vito Ghafi, Dhahabu na Madini ya Metali* | *6%* |
| *Vito vilivyokatwa (cut & polished)* | *1%* |
| *Madini ya aina nyingine (kama vile Makaa ya Mawe, Madini ya Viwandani na Madini ya Ujenzi)* | *3%* |
| *Ada ya Ukaguzi kwa madini ya aina zote* | *1%* |

***Jedwali Na. 4 Ada za Usafirishaji nje na Uingizaji Madini nchini Tanzania***

| ***Aina ya Kibali*** | ***Kutoa [USD]*** | ***Kuingiza [USD]*** |
|---|---|---|
| *Kibali cha Madini au Sampuli za Madini* | *100* | *300* |
| *Vibali Maalum vya Madini kwa Wageni* | *1,000* | *Haihusiki* |
| *Vibali Maalum vya Madini kwa Wageni wenye Visa ya Utalii* | *100* | *Haihusiki* |
| *Vibali Maalum vya Madini yaliyonunuliwa kwenye Gem Trade Fair* | *100* | *100* |

# 3.2 Kwanini uwekeze mkoani Ruvuma




**Mkoa wa Ruvuma una fursa nyingi za uwekezaji hasa kwa upande wa Sekta ya Madini. Mazingira ya Mkoa wa Ruvuma yanachochea kwa kiasi kikubwa katika kuvutia uwekezaji kwenye Sekta ya Madini. Mazingira yanayovutia uwekezaji kwenye Sekta ya Madini kwa Mkoa wa Ruvuma ni:-**

## 3.3 Upatikanaji waWafanyakazi na wachimbaji wenye ujuzi;

**Mkoa wa Ruvuma una nguvu kazi ya kutosha ya wafanyakazi wenye ujuzi na wasio na ujuzi.Wafanyakazi wenye ujuzi wapo wa kutosha kufuatia ongezeko la vyuo vingi nchini vinavyotoa mafunzo yanayohusiana na shughuli za utafiti na uchimbaji madini.**

**Mafunzo hayo kwa sasa yanatolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dar es Salaam Institute Of Technology, Chuo cha Madini Dodoma, Mbeya University of Science and Technology, Tanzania Geomological Centre, n.k**

## 3.4 Uwepo wa miundombinu ya barabara zinazopitika kwa mwaka mzima

**Mkoa wa Ruvuma upo kusini mwa Tanzania ukipaka na nchi za Msumbiji na Malawi kwa upande wa Kusini na Magharibi, mikoa ya Mtwara na Lindi kwa upande wa Mashariki na mikoa ya Njombe na Morogoro upande wa Kaskazini.**

**Nafasi ya kijiografia ya Mkoa wa Ruvuma inaupatia mkoa unafuu wa miundombinu hasa ya bandari na barabara. Mkoa wa Ruvuma upo karibu na bandari ya Mtwara ambayo inaunganisha mkoa na Dunia, pamoja na bandari nyingine ndogo zilizopo Ziwa Nyasa ambazo zinauunganisha Mkoa na nchi za Msumbiji, Malawi, pamoja na Mkoa wa Mbeya.**



**Aidha, Mkoa wa Ruvuma una miundombinu ya barabara zinazopitika kwa mwaka mzima, umeme wa kutosha na maji ya kutosha kutoka kwenye mito inayotiririsha maji mwaka mzima.**

## 3.4 Upatikanaji wa Huduma Muhimu za Jamii

**Katika kuboresha uwekezaji katika Sekta ya Madini, mkoa wa Ruvuma umehakikisha huduma muhimu za jamii zinapatikana ndani ya mkoa.**

**Huduma za jamii zinazopatikana ni pamoja na uwepo wa taasisi za fedha, huduma za afya, miundombinu ya mawasiliano, upatikanaji wa chakula cha kutosha pamoja na utulivu unaotokana na hali ya nzuri ya ulinzi na usalama.**




**Uwepo wa huduma hizo muhimu zinaweka mazingira bora ya uwekezaji katika Sekta ya Madini mkoani Ruvuma.**

# 3.5 Umilikishwaji ardhi ya uchimbaji wa madini



**Tanzania ina eneo la ukubwa wa Kilometa za Mraba 945,087 ambapo mkoa wa Ruvuma una asilimia 6.74 ya eneo hilo sawa na kilometa za mraba 63,669.Katika masuala ya ardhi, Tanzania ni moja ya nchi zenye mifumo mizuri ya umilikishwaji wa ardhi.**

**Kama inavyotamka Katiba ya nchi kuwa ardhi ni mali ya umma na Rais ndiye mdhamini kwa niaba ya raia wote, utaratibu wa kupata ardhi kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za madini na masuala mengineyo limekuwa ni jambo linalotekelezeka. Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ni mwongozo wa kitaifa kuhusu mfumo wa umiliki, matumizi na usimamizi wa ardhi.**



# FURSA ZA UWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA




**Uwekezaji katika Sekta ya Madini Mkoa wa Ruvuma ni pamoja na:-**

**Fursa zinazopatikana katika Sekta ya Madini ni uwepo wa aina nyingi za Madini yanayopatikana katika maeneo mbalimbali ndani ya mkoani Ruvuma;**

**Kushiriki katika shughuli za uchimbaji wa madini yanayopatikana katika Mkoa wa Ruvuma;**

**Kuwekeza kwenye mitambo ya *VAT leaching* na viwanda vya uchenjuaji wa dhahabu;**

**Kwekeza kwenye utoaji wa huduma za jamii katika maeneo yenye migodi inayoendesha shughuli za uchimbaji wa madini;**

**Kuwekeza kwenye ushirika na wachimbaji wadogo wenye changamoto ya mitaji;**

**Kushiriki kwa kusambaza teknolojia rahisi kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini hasa uchimbaji mdogo;**

**Kushirika katika biashara ya madini kwa kutumia leseni za biashara kubwa (dealer) ama biashara ya udalali ndogo (broker);**

**Kushiriki katika shughuli za kuongeza thamani ya madini mfano kukata na kusanifu madini ya vito;**

**Kuwekeza kwenye usafirishaji wa makaa ya mawe ambayo ni moja-wapo ya madini yanayochimbwa kwa wingi mkoani Ruvuma;**

**Kuwekeza kwenye vifaa na zana zinazotumika kwenye uchimbaji wa madini mfano baruti na mitambo;**